

NIKITAFAKARI NAOGOPA

Tafakari

Music by: Byabato

1. Ni ki ya ta fa ka ri ma te ndo ya ko Bwa na, na o go pa mi mi na o go pa.
Ni na po ya ku mbu ka maa ja bu ya ko Bwa na, na o go pa mi mi na o go pa.

(KI - NA - NDA) U li vyo zi u mba mbi ngu, na vyo te vi li vyo mo,

u li vyo i u mba n chi, na vyo te vi li vyo mo, U ka i we ka n chi

chi ni ya mwa na da mu, pa mo ja na ki bu ri, ba do u li m kwe za,

{Chorus}

15

Ha ku na, ka ma - we we

ha ku na ka ma we we Mu ngu. a li ye ka ma, Mu ngu we

19

ha ku na ka ma we we Mu ngu,

tu ha ku na ka ma we we - Mu ngu,

2. Ninapotafakari Sodoma na Gomora, naogopa mimi naogopa;
 Ninapozikumbuka nyakati zake Nuhu, nao gopa mimi naogopa;
 Ulivyowaadabisha, watendao maovu, huku ukiwahifadhi wakutumikiao;
 Na ukawakusanya, kama taifa moja, uka-wapandisha, kwenye mlima wako;
 Hakuna kama wewe Mungu: Hakuna

3. Ninapotafakari ile fimbo ya Musa, naogopa mimi naogopa,
 Ninapoyakumbuka mapigo kwa Farao, naogopa mimi naogopa,
 Ulivyogeuzi maji, yakawa damu tupu, tena ukaigauza, bahari nchi kavu;
 Kisha ukawavusha, wana wa Israeli, na ukalizamisha, jeshi lake Farao;
 Hakuna kama wewe Mungu: Hakuna

4. Ninapotafakari ujio wa Mwanao, naogopa mimi naogopa,
 Ninapoikumbuka miujiza aliyotenda, naogopa mimi naogopa,
 Aliwafufua wafu, na kuponya wagonjwa, lakini taifa lake, hawakumsadiki;
 Yakuwa ndiye Kristu, na mkombozi wetu, uliye mtuma kuja, kutukomboa sisi;
 Hakuna kama wewe Mungu: Hakuna